



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI RUFJI



Kumb. Na. HA.80/118/01/53

Tarehe 25 Oktoba, 2025

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Rufiji anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi (04) katika Halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

1.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II - NAFASI 04

1.1 MAJUKUMU NA KAZI

- i. Kuorodhesha barua zinzoingia masijala kwenye rejista(Incoming correspondence register)
- ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi(Outgoing Correspondance Register).
- iii. Kusambaza Majalada kwa watendaji(Action Officers)
- iv. Kupokea Majalada yanayorudi masijala kutoka kwa Watendaji
- v. Kupokea majalada na kusambaza kwa Maofisa walio katika Idara/Kitengo/Sehemu husika
- vi. Kutafuta kumbukumbu/Majalada/Nyaraka zinazohitajika kwa watendaji.
- vii. Kurudisha Majalada kwenye shubaka/Kabati la majalada(Racks/filling Cabinets) au mahala pengine yanapohifadhiwa.
- viii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani na nje ya Taasisi(File Tracking)

1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha Nne au Sita wenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au cheti cha NTA Level 6 katika fani ya Utunzaji wa kumbukumbu kutoka katika vyuo vinavyotambulika na Serikali pamoja na ujuzi wa kutumia kompyuta.

1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA

TGS C

MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii. **Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira Ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya ajira katika Utumishi wa Umma.**
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na anuani ya barua pepe (E- mail Address) pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika
Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificate – Cheti cha Mtihani wa Kidato cha nne na cha Sita, Computer Certificate, - Vyeti vya Kitaaluma (Professional Certificate from Respective Boards).
- v. Wasailiwa watakaowasilisha **Testimonials, Provisional Results, Statement of results, hatiza matokeo za kidato cha IV na VI (form V and form VI results slips) HAVITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI.**
- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika **(TCU, NECTA na NACTVET).**
- vii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

- viii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika **Waraka Na. CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**
- ix. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.
- x. Wasailiwa ambao majina yao yanatofautiana katika nyaraka zao wanapaswa kuwasilisha Hati ya Kiapo cha Kubadili Jina (Deed Poll) iliyosajiliwa na Wizara ya Ardhi.
- xi. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **08 Desemba, 2025**
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Mji,
S.L.P 28,
UTETE/RUFIJI
- xii. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz> (Anuani hii pia inapatikana kwenye Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa “Recruitment Portal”)
- xiii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili
HAYATAFIKILIWA
Limetolewa na:

MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI WA RUFJI